**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS- TAMISEMI**

**HALMASHAURI YA MJI MAKAMBAKO**

SHULE YA SEKONDARI MTIMBWE,

S.L.P 75,

**MAKAMBAKO.**

TAREHE ................................

**Namba za simu.**

**Mkuu wa shule:** 0752648114/0623530211

**Makamu wa mkuu wa shule** 0754981377

**Ndugu**

Mzazi/mlezi wa ..........................................................................................

YAH: **MAAGIZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO SHULE YA SEKONDARI MTIMBWE, HALMASHAURI YA MJI MAKAMBAKO, MKOA WA NJOMBE, MWAKA 2023/2024.**

1. Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha Tano (V) katika Shule ya sekondari Mtimbwe ambayo ipo Halmashauri ya Mji Makambako umbali wa kilometa 22 kutoka Makambako mjini barabara ya kuelekea Njombe, na tahasusi zilizopo shule hii ni HGL na HGE. Namna ya kufika shuleni ukishashuka Makambako Mjini utapanda mabasi yanayoelekea Njombe na utashukia Ikelu **(Nauli ni tsh 2000/=).** Utapanda pikipiki / bodaboda hadi shuleni **(Nauli tsh 2000).**

   Muhula wa masomo unaanza tarehe 14/08/2023 hivyo basi mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe 13/08/2023: na mwisho wa kuripoti ni terehe 30/08/2023. Hatua za kinidhamu zitachukuliwa kwa atakaye chelewa kufika shuleni.

2. **KAULIMBIU YA SHULE/SCHOOL MOTTO "EDUCATION FOR THE BRIGHT FUTURE"**

   Kauli hiyo ndiyo dira yako utakapokuwa hapa kwa kipindi chote cha miaka miwili. Unatakiwa kuitafakari na kuitekeleza kauli hiyo kwa vitendo. Ni matumaini yetu kuwa utatumia nafasi hii adimu kwa manufaa yako na Taifa kwa ujumla. Hivyo basi, utatakiwa kuwa na tabia njema na uhudhurie masomo na ujifunze kwa bidii.

..............................................

**ZUBERI J. KILINGO**

**MKUU WA SHULE.**

## 3. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

### 3.1 SARE ZA SHULE

a) Suruali mbili (2) za **khaki aina ya esteem** zenye mifuko miwili mbele na nyuma mmoja upana miguuni ni inchi 16 na linda mbili kila upande (dats) na mkunjo wa chini ukunjwe kwa nje (**"turn up"**) inchi moja (1) na si vinginebyo.
b) Mashati meupe mawili ya mikono mirefu (tetroni)
c) Tai za khaki mbili
d) Sweta mbili rangi ya **chocolate** yenye mshono wa **" V**"
e) Soksi nyeusi jozi mbili
f) Fulana nyeupe jozi mbili
g) Mkanda mweusi wa kuvalia suruali ( usiwe na urembo, pia chuma kinene kupita kiasi)
h) Viatu vya ngozi nyeusi visivyo na kisigino kirefu jozi mbili vya kufunga na kamba (**gidamu)**.
i) Track-suit nyeusi yenye mistari myeupe isiyo na kofia.
j) T-shirt mbili za blue bahari zenye kola shingoni **(aina ya form six)**.

**Angalizo:**

**i) Mwanafunzi anapokuja shuleni awe amevaa tracksuit au sare za shule zilizoagizwa hapo juu.**

### 3.2 VIFAA VYA DARASANI

a) Daftari za kutosha (**counter books 7 za quire 4**), Kalamu za kutosha (**blue pen or black pen na penseli**),Scientific calculator (**kikokotozi**) kwa wanafunzi wa **HGE.**
b) Mkebe **(mathematical set**) na Saa ya mkononi.
c) Graph paper pad, kwa matumizi yake darasani.
d) Bunda mbili za karatasi (**ream A4**) kwa mwaka.
e) Vitabu vya masomo husika (orodha imeambatanishwa kwenye fomu hii).
f) Folder file.

### 3.3 . VIFAA VYA BWENINI

a) Ndoo mbili (02) za lita kumi (10) zenye mifuniko kwa matumizi ya mwanafunzi.
b) Godoro moja (01) futi 2.5 kwa sita.
c) Mto mmoja (01) na foronya rangi ya blue bahari.
d) Shuka mbili (02) rangi ya blue bahari.
e) Blanketi moja (01)
f) Chandarua (01)
g) Taulo
h) Ndala
i) Mswaki na dawa ya mswaki.
j) Sanduku (trunker (01) imara la bati lenye makufuli kwaajili ya kuhifadhia vitu vyake.

**VIFAA VYA USAFI**

HGE

i. Jembe lenye mpini moja (01)
ii. Mopa (Draya) moja (01) yenye mpini.
iii. Brashi ngumu (hard broom) moja (01)yenye mpini.
iv. Fagio (chelewa )01

HGL

i. Fagio laini la kufagilia ndani (soft broom) yenye mpini moja (01)
ii. Fyekeo moja (01)
iii. Mopa (Draya) moja (01) yenye mpini.
iv. Fagio (chelewa )01

### 3.4 VIFAA VYA CHAKULA

i. Kikombe – 01
ii. Sahani -01
iii. Bakuli -01
iv. Kijiko -01

### 3.5 SARE ZA MICHEZO

Mwanafunzi aje na **bukta moja na T-shirt (jezi -01) moja** ya michezo kwa mchanganuo wa rangi kama ifuatavyo;-

i. HGL – Jezi nyeusi, mistari myeupe na kiatu cha michezo.
ii. HGE - Jezi ya blue yenye mistari myeupe na kiatu cha michezo.

### 3.6 SARE ZA KUSHINDIA (SHAMBA DRESS)

a) Suruali nyeusi mbili za kitambaa kwa ajili ya sare ya kazi/shughuli za nje ya darasa mshono wa suruali iwe zenye mifuko 2 mbele na nyuma mfuko mmoja upana mguuni ni inchi 16 na linda mbili kila upande (dats) na upindo wa chini miguuni ugeuzwe juu (turn up)
b) Koti (jacket) moja(01) jeusi lisilo na maandishi/maua kwaajili kujikinga na baridi

NB: Suruali nyeusi na T-shirt ni kwa ajili ya kushindia(form six). ***Suruali za mitumba na jeans haziruhusiwi hapa shuleni.***

### 3.7 MAHITAJI BINAFSI

- Aje na fedha za kumtosha kwaajili ya matumizi yake binafsi akiwa hapa shuleni.
- Vifaa vyote vilivyoagiza vitakaguliwa katika ofisi ya usajili kabla ya mwanafunzi kusajiliwa.
- Vifaa vya shule na mahitaji binafsi vinaweza kununuliwa kwenye maduka yaliyopo karibu na shule ili kumpunguzia changamoto kwenye usafiri.
- Masomo yanayofundishwa (A-level ) ni;-

i. HISTORY
ii. ENGLISH
iii. GEOGRAPHY
iv. GENERAL STUDIES (G.S)
v. BASIC APPLIEC MATHEMATICS (BAM)
vi. ECONOMICS.

### 3.8 ADA NA MICHANGO MBALIMBALI YA SHULE

| S/N | MCHANGO | KIDATO CHA TANO | KIDATO CHA SITA |
|---|---|---|---|
| 01 | Mchango wa samani | 20,000 | - |
| 02 | Kitambulisho na picha | 6,000 | - |
| 03 | Nembo ya shule | 2,000 | - |
| 04 | Ukarabati wa samani | 20,000 | 20,000 |
| 05 | Tahadhari (caution money) haitarejeshwa | 5,000 | - |
| 06 | Wapishi, walinzi na vibarua (kwa mwaka) | 30,000 | 30,000 |
| 07 | Huduma ya kwanza (First Aid) | 5,000 | 5,000 |
| 08 | Mtihani wa MOCK | - | 20,000 |
| 09 | Pre- Necta examination | - | |
| 10 | Stampu na bahasha | 5,000 | - |

**ANGALIZO:**

(i) Ada ya mtihani wa Taifa (NECTA) kwa kidato cha sita, italipwa kulingana na maelekezo ya viwango vya wakati huo kutoka mamlaka husika.

(ii) Jumla ya Ada na michango mingine kwa kidato cha tano ni **shilingi 93,000/=**

### 3.9 UTARATIBU WA KULIPA MICHANGO.

**S**hule haipokei fedha taslimu au hundi kutoka kwa wazazi / walezi wa wanafunzi na badala yake malipo yote yaliyoainishwa kwenye jedwali hapo juu yalipwe kupitia **BENKI YA NMB (National Microfinance Bank)** kwenye tawi lolote Tanzania lililopo karibu nawe kabla ya kuja shuleni.

Jina la akaunti ya shuleni : **MTIMBWE SEKONDARY SCHOOL EK.**

Namba ya akaunti : **60310020811 NMB.**

**Tafadhari andika jina la mwanafunzi na tahasusi yake kwenye pay in slip na uiwasilishe kwa mhasibu wa shule pindi ufikapo shuleni kwa uthibitisho zaidi.**

**.......................................**

**ZUBERI J. KILINGO**

**MKUU WA SHULE**

**4. SHERIA ZA SHULE**

Shule inaendeshwa kwa **mujibu wa sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978**, kama ilivyorekebishwa **kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995**. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, yenye dhamana ya Elimu Nchini na **Ofisi ya Rais- TAMISEMI,** yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa Elimu.

Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa, kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.

a. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.

b. Kuwahi kufika shuleni na kuwa mstarini saa 1:00 asubuhi.

c. Kuhudhuria shuleni siku zote na muda wote wa masomo.

d. Kuhudhuria vipindi vyote vya masomo ndani na nje ya darasa ikiwemo vipindi vya dini kila wiki.

e. Kuhudhuria kazi zote za mikono.

**f.** Kuhudhuria mikutano ya shule. **Mfano;- Baraza la shule , ukaguzi wa usafi, kupandisha Bendera ya Taifa, vikao vya madarasani** na vikundi mbalimbali vinavyotambulika kisheria; **mfano; Vilabu vya masomo, Dini, Utamaduni, maadili nk.**

g. Kuitika miito ya dharula mara moja.

h. Kushiriki kuimba wimbo wa Taifa wakati wa kupandisha Bendera ya taifa pamoja na nyimbo nyingine za kizalendo.

**i.** Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule **(Mwanafunzi haruhusiwi kufuga kucha ndefu, na nywele ndefu au kunyoa kipara)**

j. Kila mwanafunzi anatakiwa ahudhurie maandalio ya jioni (preparation ) kuanzia saa 07:30 jioni hadi saa 10:00 usiku.

k. Ni **LAZIMA** mwanafunzi awe katika sare ya shule na **KITAMBULISHO** kwa nyakati zote awapo shuleni na nje ya shule. **Mfano**; Anapotoka nje ya shule kwa ruhusa maalumu, **kwenda posta, kanisani, msikitini,Benki,Hospitali, Likizo** au kwa shughuli yoyote itakayokulazimu kwenda nje ya shule.

l. Kuzingatia ratiba ya Shule wakati wote (Uwe mahali sahihi kwa wakati sahihi)

m. Kutunza mali ya umma.

**n.** Ni marufuku kwa mwanafunzi kumiliki **SIMU** ya mkononi , **LAINI** ya simu ya mkononi au **CHAJI** ya simu ya mkononi na endapo ataonekana kumiliki vitu hivi tajwa hapo juu **Mwanafunzi atafutwa shule.**

o. Kukataa adhabu ni kukataa malezi bora ya walezi wako wa shule, maana yake ni kukataa kuwa mwanafunzi wa shule hii.

p. Kuchochea au kusababisha mgomo wa aina yoyote shuleni ni marufuku na haramu.

q. Kuvaa nguo za mitindo. **Mfano; Model**.

r. Wageni wa mwanafunzi wataruhusiwa kuonanana naye baada ya kujitambulisha na kupokelewa na mwalimu wa zamu.

s. Mwanafunzi atajisafirisha mwenyewe wakati wa likizo au pale atakaporudishwa nyumbani/ kufukuzwa shule.
t. Mwanafunzi atafuata maelekezo yanayotolewa mara kwa mara na uongozi wa shule.
u. Hairuhusiwa mwanafunzi yeyote kwenda katika nyumba za walimu bila ruhusa kutoka kwa mwalimu.
v. Mwanafunzi haruhusiwi kuoa wakati akiwa bado mwanafunzi: akibainika atafukuzwa shule mara moja. Aidha ni marufuku kuwa na uhusiano wa kimapenzi awapo mwanafunzi.
w. Ni **LAZIMA** mwanafunzi awe ndani ya mipaka ya shule wakati wote isipokuwa akiruhusiwa kuwa nje ya mipaka ya shule kwa ruhusa maalumu na atapaswa kuwa na kibali **(GET PASS)** cha maandishi.
x. Ni marufuku kuvaa/ kuja na mavazi kinyume na yaliyoagizwa.
y. Mwanafunzi haruhusiwi kumiliki kamera au komputa mpakato **(LAPTOP)** shuleni.
z. Kuwa mfano mwema ndani na nje ya shule.

NB: “**Shule haitamvumilia mwanafunzi atakayevunja kanuni hizo hapo juu”.**

## 5. MAMBO YAFUATAYO YATASABABISHA UFUKUZWE SHULE..

a. Kudharau Bendera ya Taifa , Picha za viongozi wa Taifa, Nembo ya Taifa, wimbo wa Taifa na fedha ya Taifa.
b. Wizi
c. Mwanafunzi kumiliki SIMU YA MKONONI au LAINI YA SIMU ya mkononi na vitu vyote vinavyotumia umeme mfano: **heater, pasi, jiko** nk.
d. Kushirikiana kuendeleza imani za kishirikina.
e. Kunyanyapaa na uonevu wa aina yoyote .
f. Kukataa adhabu kwa makusudi.
g. Kuoa.
h. Uasherati, ubakaji, ushoga, ulawiti na usagaji.
i. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya , uvutaji sigara na biashara na madawa yote ya kulevya.
j. Makosa mengine ya jinai.
k. Kugoma na kuhamasiha mgomo.
l. Kupiga au kupigana na mwanafunzi mwenzake au mtumishi.
m. Kuharibu mali ya umma nay a watu wengine.
n. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu / walezi na jamii kwa ujumla.
o. Kugoma, kuchochea au kuongoza kuvuruga amani na usalama wa watu shuleni.
p. Kushiriki matendo ya uhalifu, na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi.
q. Kusababisha mimba au kumpa mimba msichana ndani na nje ya shule.
r. Kujiachisha shule mwenyewe.
s. Kufanya jaribo lolote la kujiua au kutishia kujiua kama kunywa sumu, dawa nk.
t. Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni.
u. Kushiriki kutoa mimba.

## MAMBO MENGINE YA MUHIMU ANAYOPASWA KUKAMILISHA NA KUWASILISHA SHULENI.

a. Cheti cha kuzaliwa.

b. Result slip.
c. Kutokana na umuhimu na gharama za matibabu kuwa kubwa tunashauri kuwa kama mwanafunzi ana bima ya afya aje nayo na kama hana mzazi/mlezi unashauriwa umkatie bima ya afya.

*FOMU NA.3*

6. **KUKUBALI / KUKATAA NAFASI**

**A: MWANAFUNZI**

1. Jina kamili **(matatu)** ..........................................................................................................
2. Shule ya sekondari uliyosoma **(O-level)** ..............................................................................
3. Namba ya Mtihani ..........................................................................................................
4. Tarehe ya kuzaliwa ..........................................................................................................
5. Nakubali nafasi niliyopewa / siikubali , apewe mwingine **(kata neno lisilohusika)** .
6. Nakiri / naahidi nitajibadilisha katika Taaluma, Nidhamu, Elimu ya kujitegemea na michezo, pia kutomiliki simu au laini; wala chombo kinachotumia umeme shuleni, kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai kama ilivyoainishwa katika sheria za shule.
7. Sahihi ................................................................ Tarehe ..................................................

**B: MZAZI/ MLEZI**

Mimi ............................................................ mzazi / mlezi wa .................................................. Nimesoma kwa makini maagizo ya mwanangu kujiunga na Shule ya sekondari Mtimbwe : Naahidi kumtimizia mwanangu maagizo yote na pia nitashirikiana na walimu katika kulea mwanangu kinidhamu ili apate taaluma inayokubalika na endapo nitazembea nihesabiwe kuwa nimegoma kumpa malezi mwanangu na nichukuliwe hatua zinazostahili.

Jina la mzazi/ mlezi ..........................................................................................................

Anuani ..........................................................................................................................

Kijiji / mtaa ..................................................................................................................

Sahihi ya mzazi/ mlezi ......................................................................................................

Namba ya simu ..............................................................................................................

Tarehe ...........................................................................................................................

**C. AFISA MTENDAJI KATA/ KIJIJI/ MTAA.**

Jina ........................................................................ Kijiji/Kata ....................................... Wilaya ...................................... Mkoa ................................... nathibitisha kuwa mwanafunzi ..................................................................... ni wa Kijiji / Kata hii na Ni raia wa Tanzania/Si raia wa Tanzania.

Sahihi .................................................. Muhuri ................................. Tarehe .......................

....................................

**ZUBERI J. KILINGO**

*FOMU NA. 4*

**A: TAARIFA BINAFSI ZA MWANAFUNZI (Ijazwe na mwanafunzi)**

1. Jina la mwanafunzi (matatu) ........................................................................................
2. Kidato cha ..................................... tahahusi ya .................................................
3. Mahali ulipozaliwa ........................................................................................
4. Tarehe ya kuzaliwa ........................................................................................
5. Jinsia ........................................................................................................
6. Umri ........................................................................................................
7. Anwani ya nyumbani ........................................................................................
8. Anwani ya mzazi/ mlezi (kama tofauti na hapo juu) ..........................................
9. Jina la mzazi/mlezi ........................................................................................
10. Dini ........................................................................................................
11. Kidato ulichopokelewa ........................................................................................
12. Shule ya sekondari uliyomaliza ........................................................................................
13. Shule ya msingi uliyomaliza darasa la saba .............................................................
14. Shughuli unazopendelea mbali na masomo, kwa mfano; mpira wa miguu, mpira wa mikono, riadha, unaimba nk. ........................................................................................
15. Wilaya unayotoka ................................................kata ...................................mtaa .....................
16. Nikihama nitatoa taarifa ........................................................................................
17. Mimi ........................................................................................ nakiri taarifa nilizotoa ni sahihi.

Sahihi ya mwanafunzi ............................................................... tarehe ...................................

NB: ***ENDAPO MWANAFUNZI ATATOA TAARIFA ZISIZO SAHIHI ATACHUKULIWA HATUA ZA KINIDHAMU.***

B: **AFISA MTENDAJI KATA /KIJIJI/MTAA.**

Jina ........................................................................ Kijiji/Kata ............................................ Wilaya :............................................... Mkoa ........................................................................

Nathibitisha kuwa mwanafunzi ........................................................... ni wa kijiji/kata hii ni raia wa Tanzania/Si raia wa Tanzania.

Sahihi .............................................. Muhuri ............................................ Tarehe........................

.................................

**ZUBERI J. KILINGO**

**MKUU WA SHULE**

***FOMU NA. 5***

**VITABU VYA MASOMO HUSIKA**

**A. HISTORY**

| S/N | AINA YA KITABU | MTUNZI |
|---|---|---|
| 01 | Major events in Africa | Kamara |
| 02 | Modern world history | Ben Walsh |
| 03 | African in the world history | Nyirenda |
| 04 | Mastering advanced level history paper 1&2 | By move as publishers and suppliers mwanza. |
| 05 | Contemporary historical events advanced level | Shibitaki Ck.Tumain (2013) |

**B. GEOGRAPHY**

| S/N | AINA YA KITABU | MTUNZI |
|---|---|---|
| 01 | General Geography in diagrams | R.B.Bunnett |
| 02 | Principal of physical Geography | F.J .Monk House |
| 03 | Plactical Geography for Africa | P. Richard |
| 04 | Land forms for Africa | Collin Bakor |
| 05 | Stastical methods and the geographer | S. Gregory |
| 06 | Certificate physical and human geography | Goh Chang Leong |

**C. ECONOMICS**

| S/N | AINA YA KITABU | MTUNZI |
|---|---|---|
| 01 | Introduction to positive economics | Lipsey |
| 02 | Economics planning and economics growth | Brech R. |
| 03 | Contemporary economics theory and practice | Wgura |
| 04 | Descriptive economics 2nd edition | |
| 05 | Economics professional studies paper one | Ambilikile |

**D. ENGLISH**

| S/N | AINA YA KITABU | MTUNZI |
|---|---|---|
| 01 | English for Advanced level | Dr. M. Kadeghe |
| 02 | Advanced English dictionary | Oxford University |
| 03 | Selected poem from East Africa | TIE and others poems text books |
| 04 | I will marry when I want | Ngugi wa Thiong'o |

**E. BASIC APPLIED MATHEMATICS**

| S/N | AINA YA KITABU | MTUNZI |
|---|---|---|
| 01 | Basic applied mathematics | TIE |
| 02 | Pure mathematics 1 and 2 | Bank house |

| | | |
|---|---|---|
| 03 | Core course mathematics | Bostoch and Chandler |

*FOMU NA. 6*

**GOVERNMENT OF TANZANIA**
**REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION**
**(FOMU YA UCHUNGUZI WA AFYA)**

**PART A;** DATE ;..............................................

FROM ..........................................
..........................................
..........................................

**TO; REGIONAL/DISTRICT MEDICAL OFFICER,**
P.O.BOX ....................................
......................................................

Mr/Mrs/miss .............................................................. Age;........................ Sex................ Height..................
*(Name in full)*

Pleased examine the above named as to his physical and mental fitness for a full – time, Advanced Level of Secondary Education.

The Examination should include the following ineligible in case of a defect.

a. E i. A
ye – sight ........................................ bdomen .....................................
b. Hj. U
earing (Ears) ................................. rine for plamotest .........................
c. L k. S
imbs ............................................. yphilis test ....................................
d. S l. B
peech ........................................... lood group ..................................
e. V m. B
eneral diseases ............................ lood count (Red &White)................
f. S n. E
tool examination ........................... pilepsy ..........................................
g. T o. L
B test ............................................ eprosy...........................................
h. S
pleen ............................................

2. Neurons

3. Other serious disease

**PART B. MEDICAL CERTIFICATE (***To be completed by government Officer)*

I have examined the above –named and consider that he/she is physical fit/unfit and mentally fit/unfit for full – time student.

a. E e. V
ye – sight ........................................ eneral diseases ............................
b. Hf. S
earing (Ears) ................................. tool examination ...........................
c. L g. T
imbs ............................................. B test ............................................
d. S h. S
peech ........................................... pleen ............................................

i. Abdomen .....................................
j. Urine for plamotest .........................
k. Syphilis test ....................................
l. Blood group ...................................
m. Blood count (Red &White)................
n. Epilepsy ..........................................
o. Leprosy ...........................................

2. Neurons

3. Other serious disease

**ADDITIONAL INFORMATION**

If any eg. Physical impairments infection, chronic or family disease ....................... ...................................... ......................................................................................................................................................................................... .........................................................................................................................................................

**I CERTIFY THAT THE ABOVE IS FIT TO PURSUE FURTHER STUDIES IN EDUCATION.**

Station .............................................................. Name .......................................................Signature .............................

Date ............................................... Designation ...................................... Official stamp...........................................

*FOMU NA. 7*

**TAARIFA ZA NDUGU WATAKAO FIKA NA KUSIKILIZA SHIDA MBALIMBALI ZA MWANAFUNZI.**

A; JEDWALI LINALOONYESHA NDUGU WA MWANAFUNZI NA PICHA ZAO ZIWEKWE HAPO CHINI.

| **Na.** | **Jina** | **Jinsi** | **Anwani yake** | **Uhusiano** | **Kabila** | **Anakotoka** | **Namba ya simu** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 01 | | | | | | | |
| 02 | | | | | | | |
| 03 | | | | | | | |
| 04 | | | | | | | |

Habari nyinginezo ;

.........................................................................................................................................................................
.........................................................................................................................................................................
.........................................................................................................................................................................

Sahihi ya mwanafunzi ........................................................................ Tarehe ............................................................

B: **MZAZI AWAIDHINISHE HAO NAO NDUGU WA MWANAFUNZI.**

Mimi ......................................................................... mzazi/mlezi wa mwanafunzi ........................................................ Ninawaidhinishia watajwa hapo juu ni ndugu wa mwanangu na watakuwa wakifika kumwona na kusikiliza shida mbalimbali wakati ambao mimi kama Mzazi/mlezi nitakuwa nimeshindwa kufika.

Sahihi ................................................. Namba ya simu ...................................................... Tarehe .............................

**C. KIONGOZI WA SERIKALI YA MTAAA/KIJIJI ATHIBITISHE TAARIFA HII.**

Mimi .................................................... Cheo ................................................. Kijiji/Mtaa ...........................................

Nathibitisha kuwa watajwa hapo juu wameteuliwa na Mzazi/Mlezi wa mwanafunzi.....................................................na

Ninakuomba uwapokee wawe walezi mbadala wa mwanafunzi tajwa hapo juu.

Sahihi ............................................ Mhuri ..................................................... Tarehe .........................................

***FOMU NA. 8***

## AHADI /KIAPO CHA MWANAFUNZI.

Mimi ......................................................................... ambaye nimechaguliwa kujiunga na SHULE YA SEKONDARI MTIMBWE KIDATO CHA TANO, MCHEPUO WA .................................... mwaka 2023/2024, ninaipokea na kuikubali nafasi niliyopewa kwa malengo ya kusoma kwa bidii na kufikia malengo ya Taifa na shule ya Sekondari Mtimbwe. Ninatambua kuwa nafasi hii ni adimu, nyeti nay a upendeleo kwangu ili niweze kusoma na kufanya vizuri katika masomo nikiwa na tabia na mwenendo mwema kwa ajili ya Taifa langu la Tanzania, familia yangu na kwaajili yangu pia.

Nina amini kuwa vitendo vyovyote vinavyopelekea uzembe katika kufanikisha makusudio haya ni hujuma kwa Taifa langu, familia yangu na kwangu pia.

Hivyo ninaahidi kuwa, nikiwa hapo shuleni;-

i. Nitasoma kwa bidii kwa malengo ya kufanya vizuri katika masomo niliyochaguliwa kusoma.
ii. Nitajihusisha na kufuata sheria na taratibu zote za shule kama nilivyozisoma na kuzielewa na zingine zitakazokuwa zikitolewa mara kwa mara.
iii. Sitajihusisha na vitendo vyovyote vya utovu wa nidhamu nikiwa hapo shuleni.
iv. Ikiwa nitakiuka sheria, kanuni na taratibu za shule kama nilivyozisoma , na kuzielewa, nitakubali kurudi nyumbani kumwita mzazi/mlezi wangu...................................................................(Jina la mzazi/mlezi) kwa hatua zaidi.

Sahihi ya mwanafunzi ...................................................................... Tarehe ..............................................

...................................

**ZUBERI J. KILINGO**

**MKUU WA SHULE**